Vital Strategies | Bloomberg Philanthropies | DATA FOR HEALTH INITIATIVE

# Mpango wa Usajili wa Saratani

Kushirikiana na serikali kuimarisha usajili wa wagonjwa wa saratani unaolingana na idadi ya watu ili kuwezesha udhibiti wa saratani.



**Saratani ilisababisha vifo vya watu milioni 10 mwaka 2020, idadi hii ikiwa karibu kifo cha mtu mmoja kati ya sita; asilimia sabini ya vifo hivyo hutokea katika nchi zenye uhaba wa rasilimali.**

Usajili wa saratani, ambazo hufuatilia data za saratani, ni msingi wa udhibiti wa saratani lakini kwa muda mrefu hazijaundwa katika nchi ambazo kwa sasa zimeorodheshwa katika viwango vya chini au vya kati vya kipato. Bila ufahamu wa mielekeo ya sasa ya saratani na makadirio ya siku zijazo, nchi haziwezi kufanya maamuzi sahihi kuhusu mikakati ya kuzuia, kugundua mapema, kufanya udhibit wa kimatibabu au utunzaji kwa watu ambao hawawezi kutibiwa. Data sahihi inahitajika ili kuhakikisha mipango na tathmini ya shughuli za kudhibiti saratani katika kila nchi duniani zimefanywa.

Mpango huu wa Usajili wa Saratani, unaojumuishwa chini ya mpango wa "Bloomberg Data for Health", hushirikiana na wizara za afya na washirika wake kuanzisha, kuimarisha na kupanua usajili wa saratani zinazolingana na idadi ya watu na kutumia data hiyo kutunga sera.

Mpango wa Usajili wa Saratani husaidia nchi kuanzisha na kuimarisha usajili wa saratani zinazolingana na idadi ya watu ili kufuatilia data za saratani, ambazo zinawezesha nchi kuelewa vyema uzito wa magonjwa ya saratani yaliyo nchini mwao na kuchukua hatua stahiki.

Ushirikiano wa kila nchi huzingatia mlengo wa kuimarisha usajili uliopo, kuunda usajili mpya unapohitajika, na kutoa usaidizi wa kitaalam na shughuli za mafunzo. Lengo letu ni kuendeleza mfumo endelevu wa usajili ili kuimarisha upangaji unaowezeshwa na data, ikijumuisha kuwezesha shughuli za kudhibiti na kuzuia saratani, kuweka vipaumbele na upangaji bajeti, pamoja na uundaji wa sera.


| ENEO LENGWA | MATOKEO |
|---|---|
| **1. Miundombinu na wafanyakazi** | • Rasilimali mahususi kwa usaidizi unaoendelea wa kukusanya na kuchanganua data<br>• Kuunganisha kwenye usajili wa raia na data muhimu ya takwimu (inapowezekana)<br>• Usajili unaotegemea idadi ya watu uliopo katika katika eneo la vyanzo lililobainishwa |
| **2. Usaidizi wa kiufundi** | • Taratibu za kawaida za uendeshaji zinazolingana na maadili bora ya kimataifa<br>• Mipango ya kitaifa ya usajili wa saratani, ripoti zinazotumiwa na umma na zile za ndani, pamoja na michakato, na muunganisho kwenye mipango ya kudhibiti saratani |
| **3. Mafundisho** | • Mafunzo shirikishi, yanayolingana na matokeo mahsusi (k.m., kuandaa taarifa za matukio ya saratani na taarifa nyinginezo)<br>• Ushauri ili kuimarisha utaalamu wa ndani ya nchi |
| **4. Kuanzisha vituo shirikishi vya usajili wawagonjwa wa saratani (Afrika)** | • Kuomba usaidizi wa wataalamu wa usajili wa wagonjwa wa saratani wa Kiafrika<br>• Kukuza ushirikiano wa vituo mbalimbali ili kuwezesha kushiriki uzoefu na taarifa<br>• Mfumo wa wataalam wa Kiafrika wa kutoa usaidizi wa kataalam na kuimarisha uwezo katika bara zima |

## Washirika wetu wa Kimataifa

- Mtandao wa Usajili wa Saratani Afrika
- Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Saratani
- Kituo cha Kitaifa cha Saratani Japani
- Kituo cha kumbukumbu cha Tata

Mpango wa "Bloomberg Philanthropies Data for Health Initiative" unafadhiliwa na "Bloomberg Philantropies" huku ufadhili wa ziada ukitoka kwenye Idara ya Mambo ya nje na Biashara ya Australia.

## Mahali ambapo tunafanya




Ili upate maelezo zaidi, tembelea **vitalstrategies.org/cancer-registry/** au uwasiliane na **data4health@vitalstrategies.org**.